Toleo 42

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## MVUA ILIPOANZA KUNYESHA

Ilifika wakati katika historia ya ulimwengu ambapo Mungu aliimwaga hukumu yake na kuangamiza wanadamu wote kutokana na maovu yao ambayo yalikuwa yamekithiri. Wakati idadi ya watu ilipozidi kuongezeka, "BWANA akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote. BWANA akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo. BWANA akasema, Nitamfutilia mbali mwanadamu niliyemwumba usoni pa nchi; mwanadamu na mnyama, na kitambaacho na ndege wa angani; kwa maana naghairi ya kwamba nimewafanya" (Mwanzo 6:5-7).

Athari za dhambi ziliendelea kukithiri; kuzorota huko kukazidi kuongezeka wakati ambapo "wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu" (Mwanzo 6:1-2). Wana wa Mungu ni wale ambao walitokana na uzao wa Sethi, na ambao walikuwa na mienendo ya kumheshimu na kumtambua Mungu wa Mbinguni. Hao walianza kuoana na mabinti wa wanadamu ambao walitokana na uzao wa Kaini, watu waabudu sanamu na wasiomcha Mungu. Hivyo ndivyo ilivyo hata sasa katika ulimwengu huu mwovu, wakati ambapo watu wanaoana nje ya imani yao, wao huwa wanaoa nje ya mapenzi yake Mungu; na matokeo yake ni wao kuanguka na kuachana na mambo ya kiroho; watu ambao mbeleni walikuwa na ushirika na Mungu.

Katikati mwa uovu huo, "Nuhu akapata neema machoni pa BWANA" (Mwanzo 6:8) kwa maana yeye alikuwa mtiifu kwa mapenzi yake Mungu. Mungu akawa ni njia ya kimbilio kwa Nuhu na familia yake kutokana na maangamizi ambayo yangejiri. Ndipo Mungu akamwambia ajenge safina, kwa maana Yeye angeleta kifo kwa wote walio hai kupitia kwa gharika ya maji ambayo ingetanda kote ulimwenguni.

Nuhu alikuwa mhubiri wa haki na inaonekana alihubiri kwa wote ambao waliweza kumsikiliza kuhusiana na hukumu ya Mungu ambayo ilikuwa yaja. Huku akiwa huenda alipatana na pingamizi nyingi na kudhihakiwa, Nuhu aliendelea na kazi hiyo kwa imani, mwaka baada ya mwingine, huku akijenga safina. Ndiposa ikajiri siku ambayo baada ya safina kujaa wanyama ambao wangeokolewa, Mungu alimwagiza Nuhu, "Ingia wewe na jamaa yako yote katika safina" (Mwanzo 7:1). "Kwa maana baada ya siku saba nitainyeshea dunia mvua" (4). Ndipo hapo Mungu akaifunga safina mlango, na katika mwaka wa 600 wa maisha ya Nuhu milango ya mito na madirisha ya mbinguni yakafunguka. Kukaanza kunyesha mvua ambayo haijawahi onekana duniani. Mungu akafanya kile ambacho alikuwa amesema angefanya, na watu wote, isipokuwa tu wale waliokuwa kwenye safina, wakaangamia katika gharika hiyo ya maji kwa maana walimkataa Mungu mkuu.

Hebu waza jinsi mambo yalikuwa kwa wale ambao walikuwa wamemwona mwanaume huyo akijenga safina. Walikuwa wamesikia onyo kuhusu hukumu ijayo, wakaambiwa wampatie Mungu mioyo yao, lakini wakapuuza ujumbe huo. Lakini siku moja tone moja la mvua likaanguka kutoka kwenye mawingu. Punde si punde kukawa na mafuriko ya maji, na waabudu sanamu, wenye kuamini kwamba hakuna habari za Mungu na kwamba haziwezi kupatikana, na wote ambao wanaamini kwamba hakuna Mungu, wote waliamini ujumbe wa Nuhu—lakini kumbe wote wakawa wamechelewa.

*(Endelea katika Ukurasa 2)*



"Walikuwa wamesikia onyo . . . wakaambiwa wampatie Mungu mioyo yao, lakini wakapuuza ujumbe huo. Lakini siku moja tone moja la mvua likaanguka kutoka kwenye mawingu."


| Tahariri | Mafundisho ya Biblia: Mwisho Wakaribia | Nakala Andamizi: Wakati Unakwisha | Agizo la Dhati | Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu |
|---|---|---|---|---|
| 3 | 4 | 5-6 | 7 | 8 |

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)*

Pengine umati wa watu ulifurika hapo kwenye safina mvua ilipoanza kunyesha. "Hebu tuingie. Tufungulie mlango tafadhali. Tuokoe!" Lakini nafasi ya wokovu kutokana na kifo hicho ilikuwa imepita, mlango ukawa umefungwa. Wakati ukawa umekwisha.

Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu ndivyo itakavyokuwa wakati Yesu atakaporudi duniani ili kutuleta kwenye kiti cha hukumu cha Mungu. "Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, wasitambue, hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu" (Mathayo 24:37-39).



"Waabudu sanamu, wenye kuamini kwamba hakuna habari za Mungu na kwamba haziwezi kupatikana, na wote ambao wanaamini kwamba hakuna Mungu, wote waliamini ujumbe wa Nuhu—lakini kumbe wote wakawa wamechelewa."

2 Petro 3:6-7,10 inatufundisha kwamba kama jinsi ulimwengu ulijaa maji na watu kuangamia katika gharika hiyo, ulimwengu wa sasa utaangamizwa kwa moto na kuchomwa, wakati Bwana atakaporudi. Hakutakuwa na nafasi ya pili, hakutakuwa na wakati wa kuomba ili kupata wokovu. Huu ndio wakati ufaao wa kujiadaa kukutana na Mungu. Huu ndio wakati wa kuingia safina ya wokovu. Tunaishi katika siku za mwisho na wakati unakwisha. Yesu Kristo yupo mlangoni na ulimwengu huu umekaribia kuangamizwa, na hukumu ya mwisho ya Mungu kuingia. Wanadamu wanaishi ni kama kwamba hakutakuwa na siku ya mwisho. Ulimwengu unawakejeli watakatifu wa Mungu. Watu wanapuuza mafundisho kuhusu utakatifu na utakaso. Watu wanajitafutia maslahi yao wenyewe na kufuata tamaa zao za mwili. Dhambi na uovu umejaa ulimwenguni. Mambo yote yako karibu kuisha. Kwa kweli Mungu atamtuma Mwanawe kuleta hukumu, kama ambavyo alituma gharika ya maji.

Tunaishi katika siku za mwisho kabla ya kumwagwa kwa moto wa Mungu katika maangamizi ya mwisho ya dunia. Je, wakati Yesu akirudi wewe utakuwa umechelewa kufanya toba. Huu ndio wakati ufaao. Je, itakugharimu nini wewe kuweza kuamini? Je, utakuwa umechelewa? Wakati unakwisha. ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma; na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake. Naam. Amina.* — Ufunuo 1:7

Siku moja, siku ambayo haiko mbali sana, Bwana Yesu atapenyeza katika mawingu na malaika wake. Mara moja, kufumba na kufumbua, tarumbeta ya mwisho ikipigwa, wakati utakuwa umekwisha. Nyakati zote na dahari zote zitaisha, nao wakati, kama ambavyo tunaujua kwa sasa utakwisha, na watu wote katika vizazi vyote, walio hai na wasio hai, watakuja kwa pamoja. Kutakuwa na ufufuo wa watu wote kila mahali, na watu wote watasimama mbele ya kiti hicho kikuu cheupe cha enzi ili kuhukumiwa. Kitabu cha uhai kitafunguliwa, na sote tutahukumiwa. Watakatifu watairithi uhai wa milele huko Mbinguni na kuwa na Bwana milele, nao waovu watatupwa kwenye ziwa la moto milele.

Mzigo ambao niko nao katika nakala hii ni wa uinjilisti. Kuna ukweli ambao Roho wa Mungu anataka watakatifu na hata wenye dhambi wote kuupata: Ya kwamba wakati unakwisha.

Roho wa Mungu amenihuisha mara nyingi katika miezi kadhaa iliyopita, na ni ombi langu kwamba Roho Mtakatifu atakuguza rohoni mwako unaposoma toleo hili. Hili sio gazeti lingine tu, wala sio mafundisho mengine tu, na hata sio ujumbe mwingine tu. Huu ni wito wa kiungu wa Bwana kutukumbusha kwamba wakati katika ulimwengu huu ni mchache sana. Kuja kwa Bwana kumekaribia sana. Punde si punde Yesu anarudi.

Dhambi na ukahaba wa ulimwengu huu daima u wazi machoni pake Bwana. Kama ilivyokuwa kwa Sodomu na Gomora, hukumu ya Mungu inakaribia kufika. Basi hebu kimbia uokoe maisha yako ili upate kuokoka. Na kama tayari unamkiri Bwana, lakini hujakuwa ukimpenda na kumtumikia Mungu kwa moyo wako wote, huu ndio wakati wa kufanya mabadiliko. Nyenyekeza moyo wako kwa Mungu na uombe ili upate rehema, kwa maana, punde si punde, hakutakuwa na rehema. Wewe ambaye ulirudi nyuma, huu ndio wakati wako wa kurudi nyumbani. Usipofanya hivyo utajipata kwamba umeenda mbali zaidi na Mungu, usipoililia damu yake Yesu. Basi hebu tusijifiche kwa kutumia jina la familia yetu, historia yetu ya kikanisa, jinsi unavyofahamika na watu, au unavyoonekana mbele ya kusanyiko lako la kanisa. Hebu tuishi kwa uwazi na ukweli mbeleze zake Mungu, na kuyachunguza maisha yetu, na kuhakikisha kwamba mambo yetu yote yako sawa mbele zake Mungu wa Mbinguni.

Kwa kweli hatujui Bwana atarudi lini, na wito huu wa kurudi kwake umefanywa kwa muda wa miaka 2,000 sasa; lakini sasa kurudi kwake kumekaribia sana, hata kuliko hapo mbeleni, na wito wa Roho wa unaosema kwamba "Wakati Unakwisha" uko wazi na pia ni dhahiri. Basi hebu wewe kuwa msikivu kwa onyo hili. Usichukulie kwamba kesho lazima itakuweko. Kuna dhambi ambazo tunahitaji kutubu, dosari ambazo tunahitaji kutakaswa, mahusiano ambayo tunahitaji kurekebisha, na mioyo ambayo inahitaji kunyenyekea. Na hata ingawa lengo langu sio kupiga unyende tu kuhusu hatari zinazokuja; lengo langu kuu ni kupaza sauti ili kutoa onyo hilo kwa nguvu zake Mungu.

Basi hebu tuandae mambo yetu ili yawe sawasawa, kwa maana wakati uko karibu kukwisha. Hebu tuishi kila siku kama kwamba hiyo ndiyo siku yetu ya mwisho, kwa maana punde si punde mambo yatakuwa hivyo.

Michael W. Smith

Oktoba, 2022

*Tutembelee*

*www.thegospeltruth.org*

*ili kujiandikisha na*

*kupata jarida*

*za mbele.*

**KUSEMA KWELI NITAKUFA, LAKINI NITAKUFA LINI?**

**KUSEMA KWELI NITAKUTANA NA MUNGU, LAKINI NITAKUTANA NAYE VIPI?**

**KWA KWELINITAISHI MILELE, LAKINI NITAISHI WAPI?**



# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: Mwisho Wakaribia

**Somo la Maandiko:** *Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja.* — Mathayo 24:44

**Muhstasari:** Kulingana na Maandiko, na pia kulingana na utaratibu wa wakati wa Mungu, na hukumu zake, wakati katika ulimwengu huu unakwisha. Kuja kwa pili kwa Kristo kumekaribia sana. Basi hebu jiandaee kukutana na Mungu wako.

### I. Mfano wa Kuweka Mambo Wazi

Wanawali Kumi (Mathayo 25:1-13)

### II. Utaratibu na Wakati wa Hukumu yake Mungu

A. Adamu na Hawa—Mafuriko: ~miaka 1656
B. Mafuriko—hadi Sheria ya Musa: <900
C. Sheria ya Musa—Kifo cha Kristo: <1500
D. Kifo cha Kristo—Wakati wa Sasa: <2,000

### III. Hukumu yake Mungu

A. Luka 17:26-29 Kama ilivyokuwa siku za Nuhu.
B. Warumi 14:10-12 Sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu.

### IV. Wakati Utakwisha Ghafla

A. Ufunuo 16:15 Yesu atakuja kama mwivi.
B. 2 Wathesalonike 5:1-3 Amani na usalama; halafu uharibifu wa ghafla.

### V. Wakati Uliochaguliwa

A. Mathayo 24:36 Ni Baba tu anajua siku hiyo.
B. Matendo 17:30-31 Ameweka siku atakayohukumu walimwengu.
C. Waebrania 9:27 Tumewekewa siku ya kifo na hukumu.
D. Luka 12:16-21 "Usiku huu wa leo wanataka roho yako"

### VI. Mwisho Wakaribia

A. Warumi 13:11 "Kwa maana sasa wokovu wetu u karibu nasi kuliko tulipoanza kuamini"
B. 1 Petro 4:7 Mwisho wa mambo yote umekaribia.
C. Ufunuo 22:20 "Naam; naja upesi. Amina"


### VII. Mambo ya Mwisho

A. 2 Petro 3:3-9 Watu wenye dhihaka na uvumilivu wa Mungu.
B. 2 Petro 3:10-12 Imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani.

Tamati

*Tengeneza mambo ya nyumba yako; maana utakufa, wala hutapona.* —Isaya 38:1

## Utaratibu na Mpangilie wa Wakati wa Hukumu yake Mungu



# WAKATI UNAKWISHA



Jua hucha na kuchwa. "Mikono" ya saa huendelea kusonga mbele. Watu wanaishi maisha haya kama kwamba daima kutakuwa na kesho, kutakuwa na siku nyingine, kutakuwa na nafasi nyingine. Lakini ukweli ni kwamba, sasa tu langoni la maisha ya milele, na wakati, kama ambavyo tunaujua kwa sasa, uko karibu sana kukwisha.

## Kristo Atarudi

Yesu yuaja punde si punde, na atakaporudi ulimwengu huu utaangamizwa. Sote tutasimama katika hukumu ya Mungu, halafu tutaishi mielele Mbinguni au Jehanamu. Wakati huo hakutakuwa na kipimo cha wakati, kwa maana hakutakuweko na wakati tena. Je, wewe uko tayari kwa siku hiyo?

## Wanawali Kumi

Yesu alitoa mfano wa wanawali kumi katika Mathayo 25:1-13, kutoa onyo kuhusu kurudi kwake, jambo ambalo lilikuwa ni hakika. Kati ya hao wanawali, watano walikuwa wenye hekima, ilhali watano walikuwa wapumbavu. Wote walikuwa na aina ya utaua ndani yao wakati walipokuwa wanamsubiri bwana arusi kurudi. Watano kati yao, ambao walikuwa wamejitenga kwa kiasi fulani kwa kuachana na uovu wa ulimwengu huu, walianza kutokuwa makini. Walianza kujiachilia na kuruhusu mafuta yao kuisha. Wakaanza kuwa watu vuguvugu, na kupoteza upendo wao kwa Mungu. Roho Mtakatifu hakuwa na uhuru wa kufanya kazi ya neema maishani mwao. Ilhali wakati moja moto wa Roho Mtakatifu ulikuwa ukifanya kazi ndani yao, kutokana na mpito wa wakati na wao kutokuwa makini kwa mambo ya kiroho, moto huo ukazima. Wengi wa watu wanaojiita Wakristo katika siku zetu wako katika hali hiyo.

"Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi" (5). Bwana arusi wetu amechelewesha kurudi kwake. Hii ni kumaanisha kwamba Kristo anakawia kurudi na kwa sasa "muda wake" wa kurudi umekwisha. Wakati akichelewa hivyo wanawali walisinzia na kulala, kwa sababu ilikuwa karibu usiku wa manane. Hizi zilikuwa nyakati za giza mahali kote ambako kulikuwa hakujafikiwa na mwangaza wa mataa haya matano. Ilikuwa ni wakati wa watu kuhisi kusinzia, na wa kulala usingizi mnono. Wazo kuu la mfano huu ni kwamba sio Wakristo wote ambao watapatikana wamelala, kwa sababu kunaweza kutakuwa na wachache ambao wanamsubiri na kutarajia kurudi kwake Bwana; lakini pia kuna onyo linalotwambia tuamke na tuwe macho, huku tukijiandaa kwa kuja kwake Yesu Kristo.

"Lakini usiku wa manane, pakawa na kelele, Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki"(6). Sasa tuko karibu na usiku wa manane. Ulimwengu umezungukwa na giza la dhambi na udanganyifu, huku Mungu akitupwa nje ya maisha ya wanadamu. Watu wengi wanafuata njia za ubinafsi wao, badala ya wao kukumbatia utakatifu na uungu wa Kristo kwa mioyo yao yote. Basi wewe hebu kuwa tayari kusikia sauti ya tarumbeta katika giza hili wakati Kristo atakaporudi. Ulimwengu unaendelea kuzorota sana kwa mambo ya kiroho kwa haraka, na lisaa liko karibu kuwadia, wakati hakutakuweko tena na kitu kinachoitwa wakati.

Bwana arusi aliporudi wanawali wapumbavu waliwaomba wale wenye hekima wawagawie mafuta yao, lakini wenye hekima hawakuwa na ya ziada. Kama ilivyo kwenye mfano huu, kila mmoja wetu anawajibika kibinafsi kwa ujuzi wake wa kiroho mbele zake Mungu. Hatuna budi kumtafuta Mungu kila siku, na kuishi tukiwa tayari kwa kurudi kwake Bwana. Mfano huu unatufundisha kwamba wanawali wapumbavu walienda kujinunulia mafuta, lakini waliporudi kumbe wakapata "mlango u(sh)afungwa" (10). Wao walikuwa wameshachelewa, kama ambavyo itakuwa wakati Yesu atakaporudi. Hakutakuwa na nafasi ya kuweka mstari wa mbele mambo muhimu, wala wakati wa kuomba msamaha tena; hakutakuwa na wakati wa kurekebisha mambo ambayo yameenda mrama, wala wakati wa mtu kubadilisha mienendo yake. Sote tutakutana na Bwana kama tutakavyokuwa wakati huo. Wanawali wapumbavu


*(Endelea katika Ukurasa 6)*

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)*

walimlilia Bwana wafunguliwe mlango, kama pengine vile wenzao katika siku za Nuhu walifanya, wakati ambapo mvua ilianza kunyesha. Ndiposa Bwana akasema, "Amin, nawaambia, siwajui ninyi. Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa" (12-13).

## Mpangilio wa Hukumu

Sisi hatujahakikishiwa kwamba kutakuwa na mwaka mwingine, na pia hatujapewa uhakika kwamba kutakuweko na siku ambayo tunaita kesho. Tunapowaza kuhusu mpangilio na wakati wa hukumu zake Mungu, ni dhahiri kwamba wakati unakwisha.



Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi ilichukua muda wa miaka 1656 ndipo Mungu akamwaga hukumu yake na kuangamiza ulimwengu katika mafuriko. Miaka mia tisa baada ya mafuriko hayo, Mungu alifanya agano na watu wake na kuwapatia Sheria ya Musa. Sheria nayo ikafanya kazi kwa miaka 1500, kabla ya enzi ya Neema kuingia kupitia kwa Yesu Kristo. Na kwa sasa ni karibu miaka 2000 tangu Kristo kufa msalabani kuwakomboa wanadamu kutokana na dhambi zao.

## Je, Ni Muda Kiasi Gani Umebaki?

"Hatutapatiwa onyo lingine la kurudi kwa Kristo isipokuwa hili ambalo unalolisoma hapa. Ni jambo ambalo litatendeka mara moja bila kutarajiwa."

Kwa jumla ulimwengu wetu umemkataa Kristo, na dhambi zimejaa kote kote. Je, Mungu atasubiri muda gani kabla ya Yeye kusema, "Tosha!!?" "Na kama ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku zake Mwana wa Adamu" (Luka 17:26). Watu watakuwa wakila, wakinywa, wakioa, na kuishi maisha ya kawaida. Na wakati huo ndipo hukumu ya Mungu itakapomwagwa. Bwana atakaporudi, "Kila goti litapigwa mbele zangu; na kila ulimi utamkiri Mungu" (Warumi 14:11). Punde si punde hakutakuwa tena na wasioamini, kwa maana sote tutamwona Kristo kwa utukufu na mamlaka yake yote. Kila mmoja wetu atasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, na atawajibika mbele zake Mungu kwa ajili ya maisha yake.

## Mwisho wa Ghafla

Wakati utakwisha bila kutarajiwa, kwa maana Kristo atakuja kwa ghafla. "Tazama, naja kama mwivi. Heri akeshaye, na kuyatunza mavazi yake" (Ufunuo 16:15). Je, wewe unayadumisha mavazi yako yakiwa safi na matakatifu, ama yamejaa madoadoa ya dhambi na tamaa za kimwili? "Kwa habari ya nyakati na majira, hamna haja niwaandikie. Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, Kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula" (1 Wathesalonike 5:1-3).

Hatutapatiwa onyo lingine la kurudi kwa Kristo isipokuwa hili ambalo unalolisoma hapa. Ni jambo ambalo litatendeka mara moja bila kutarajiwa.

Hakuna mtu ajuaye siku hiyo ambapo wakati utakwisha isipokuwa Mungu mwenyewe. Hata Yesu hajui, "ila Baba peke yake" (Mathayo 24:36). Wahudumu wa Injili na makundi ya kidini wametabiri kuhusu wakati huo ambapo Bwana atarudi. Lakini hili ni jambo lisilo na maana na la kimwili, kwa maana maandiko yanafundisha kwa uwazi kwamba ni Mungu tu ajuaye ni lini. Lakini Mungu ametupatia Neno lake ambalo linatuarifu kwamba tuko katika siku za mwisho na kwamba mwisho wa mambo uko karibu sana.

## Siku Iliyotengwa

Mungu "ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki" (Matendo 17:31). Yeye ameweka wakati, na kulingana na ishara zote zilizopo, siku hiyo inakaribia kwa haraka. Hakuna mtu ambaye ataepuka miadi hiyo ya Bwana. Katika Luka 12:16-31 Yesu alitoa mfano wa tajiri mmoja ambaye alikuwa na mipango kabambe ya siku zake za usoni. Alikuwa amepanga kuvunja maghala yake na kujenga maghala mapya makubwa zaidi, ili aishi raha mustarehe na kuyafurahisha maisha yake. Lakini Mungu akanena naye: "Mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka roho yako" (20). Bwana huyu aliingia umilele wake bila kujiandaa kukutana na Mungu. Na hata kama Bwana hatakuja kutuchukua sisi sote usiku wa leo, pengine kwako wewe hii ndio siku yako. Je, unaishi hivi kwamba roho yako ikitakikana utakuwa tayari? Kamwe hauwezi kubadilisha miadi hiyo ya kukutana na Bwana.

## Kwa Kweli Mimi Naja Upesi

Wakati unakwisha. "Lakini mwisho wa mambo yote umekaribia; basi, iweni na akili, mkeshe katika sala" (1 Petro 4:7). Yesu alimshuhudia Yohana karibu miaka 2,000 iliyopita na kumwambia, "Naam; naja upesi" (Ufunuo 2:20). Je, sasa Yeye yuko wapi? Bila shaka Yeye anasubiri langoni. "Katika siku za mwisho watakuja na dhihaka zao watu wenye kudhihaki . . .na kusema, Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake?" (2 Petro 3:3-4). Muda ulikuwa umepita, lakini Petro akawakumbusha wasikilizaji wake kwamba kama vile ulimwengu wa kale uliangamizwa kwa maji, sasa huu wetu nao utaangamizwa kwa moto. Mungu ni mvumilivu na "hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba" (9).

## Kuwa Tayari kwa Kurudi Kwake

"Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa" (2 Petro 3:11). Wakati umekaribia kufika kikomo, na Kristo atarudi siku yoyote ile. Je, wewe uko tayari? Kama hauko tayari, basi huu ndio wakati wako wa kutubu na kumwomba Yesu kuingia moyoni mwako. Sasa ndio wakati wa kuandaa maisha yako kwa ajili ya siku zako za milele. Kama hauko tayari kujisalimisha leo, huenda ikawa hata kesho hutakuwa tayari kufanya hivyo. ■

# Agizo la Dhati

(Masomo ya Biblia – Bible Lessons, Vol 17 No.4, 1985)

*Leslie C. Busbee*



Kutoka kwa Petro, Paulo, na hata Yakobo tunapata utabiri kuhusu kurudi kwake Yesu. Siku zinakimbia zikielekea kwa siku hiyo kuu ya mwisho, wakati mambo haya yote yatatimia . . . Basi hebu tuwe na hakikisho kwamba Yeye atadumisha ahadi yake na kwamba atarudi tena kama ilivyotabiriwa. Yawezekana jambo hilo liko karibu sana kuliko jinsi tunavyofikiria. "Wakati wasemapo, Kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula." Mdundo wa moyo wa ulimwengu wa sasa ni wa kutafuta amani na usalama. Lakini haijalishi vile mwanadamu anajihisi salama katika ulimwengu huu mwovu wa sasa, na pia haijalishi jinsi anavyozama kwenye utajiri wa mali za kilimwengu; mambo hayo yote yataharibiwa kwa ghafla. Ulimwengu huu utaangamizwa wakati Kristo atakaporudi. Hakutakuwa na kunyakuliwa kwingine hapo katikati, au mateso mengine yenye lengo la kuwapatia watu nafasi nyingine ya kukutana na Bwana. Yesu akija, wafu watafufuliwa -- watakatifu na wenye dhambi, wazuri kwa waovu, walio wa haki na wasiokuwa wa haki. Mambo hayo yote yatafanyika kwa wakati mmoja. Yeye atakuja kulipiza kisasi kwa wote wasiomjua Mungu, na pia kupata utukufu kutoka kwa watakatifu wake. Hakutakuwa na kipindi kingine cha miaka elfu moja, toka wakati wa kufufuliwa kwa wenye haki kufikia wale waovu. Ikiwa wewe utapatikana tayari na kukubalika mbele zake, hauna budi kuwa katika hali hiyo inayofaa wakati Yesu atakaporudi. Ni lazima upatikane kwamba huna manung'uniko yote, ubishi wote, mgororo wote, kinyongo chote moyoni mwako. Litakuwa jambo muhimu sana kwetu kuhesabiwa kwamba tunafaa kusimama mbele zake Mwana wa Adamu siku hiyo kuu.

Basi mwanadamu kuwa tayari kukutana na Bwana ndio uamuzi wa dhati na shauku kuu la mtoto wa Mungu. Ni jambo linastahili kuwa kwenye mawazo yetu kila siku. Yaweza kuwa leo ndio siku yako ya kukutana naye. Mioyo yetu na mawazo yetu yanastahili kuwa mbali na ulimwengu mwovu wa sasa, na badala yake yawe yamekaziwa kwa hazina zetu ambazo ziko juu mbinguni ambako Kristo amekaa kwenye mkono wa kulia wa Mungu, huku "tukiwa na tarajio" hadi siku itakapofika ambapo Yeye atarudi tena. "Kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu" (Waebrania 9:28). Mtume Paulo anasema taji la uzima litapewa "wote pia waliopenda kufunuliwa kwake." . . . kwa kweli sisi tukimuishia kwa uaminifu na kumdumisha nambari moja katika mioyo na mawazo yetu, tutaweza kuukaribisha ufunuo wenye utukufu wakati Kristo akija kwenye wawingu ya mbinguni kwa nguvu na utukufu mkuu! Ndiposa tumeagizwa kwamba tuwe watu wanaonena mambo matakatifu na ya utauwa, na tupatikane ndani yake kwa amani, bile dosari na lawama. Hili ni agizo la dhati na himizo kuu kwetu. Yesu alitwambia katika Luka 21:36: "Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu." Je, si ni jambo njema ikiwa tutateseka kama Wakristo kwa wakati huu na kupata thawabu tutakapofika humo mbinguni! Hebu tafakari kuhusu watakatifu ambao wameondoka mbele yetu wakifufuliwa tena huku wakiwa na uhai mpya pamoja na ujuzi mpya! Mwaka unaokuja unaweza kuwa wa mwisho wa sayari hii ya kale inayoitwa Dunia. Hata kama kuja tena kwa Bwana kutakawia kwa miaka 20 ijayo, basi si hilo ni jambo lililo karibu sana kuwadia, au sio? Na kama litafanyika miaka kumi ijayo, si ni kweli kwamba limekaribia hata zaidi. Au ikiwa liko umbali wa miaka mitano, si bado liko pomoni lafika! Vipindi hivi vyote vya miaka ni mapito tu ya haraka, punde si punde vitapita. Hebu basi Bwana aongoze mioyo yetu na kutuelekeza kwa upendo wake wa kumsubiri Kristo kwa subira. ■



"Yaweza kuwa leo ndio siku yako ya kukutana naye. Mioyo yetu na mawazo yetu yanastahili kuwa mbali na ulimwengu mwovu wa sasa, na badala yake yawe yamekaziwa kwa hazina zetu ambazo ziko juu mbinguni."

JE, WAJUA?

Kuja kwa pili kwa Yesu ni somo kuu katika Agano Jipya. Ni somo ambalo limetajwa zaidi ya mara nane ikilinganishwa na jinsi kuja kwa mara ya kwanza kwa Bwana wetu kulivyotajwa. Jambo hili limeashiriwa zaidi ya mara 300 katika Agano Jipya."

(Ukweli Kuhusu Kuja kwa Pili kwa Kristo." Christian Courier. 9/20/2022).

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# KUSUBIRI KURUDI KWA BWANA KWA UVUMILIVU

*Nanyi vumilieni, mthibitishe mioyo yenu, kwa maana kuja kwake Bwana kunakaribia.*
— Yakobo 5:8

Hata ingawa dhambi imejaa katika jamii, na watu wanaendelea kudondokwa na machozi ya maisha haya, sisi kama watoto wa Mungu tuna tumaini la ajabu na utukufu, kwamba kunakuja siku bora zaidi. Kuja kwa Bwana si jambo la kuogofya kwa wale ambao wameokoka. Tunatumai ile siku ambayo Bwana Yesu atapenyeza mawinguni na kutupeleka nyumbani kwetu kwa milele huko Mbinguni. Hakutakuwa machozi tena, kuvunjika tena kwa moyo, uchungu, magonjwa, mzigo wa kuwabeba wapendwa wetu ambao hawajaokoka; tutakuwa katika uwepo wa yule ambaye alitupenda na ambaye alitoa maisha yake kwa ajili ya ukombozi wetu. Kuna wimbo usemao, "Nangojea, nina shauku kubwa kuitwa humo; wakati ule nitakuwa huru kutokana na majonzi na shida zote; wakati nitatawala na Yesu huko nyumbani kwetu mbinguni, huko nitatazama urembo wake milele."



Hiyo itakuwa siku ya ajabu sana huko Mbinguni; lakini ukweli ni kwamba bado hatujafika huko. Wakati ukijihisi mizigo ni mizito na giza la usiku linaonekana haliishi, wewe endelea kushikilia imani, kwa sababu "kuja kwa Bwana kumekaribia sana." Watu wengine wanatokomea katika majonzi ya hali zao za maisha na kupoteza tumaini lao la Mbinguni. Wengine wanajitoa kwa falsafa na misukumo ya ulimwengu ulioanguka, na kupoteza ari waliyokuwa nayo ya kufuata makusudi yake Mungu maishani mwao. Ilhali wengine huruhusu imani yao kufifia inapozongwa na athari na giza la maisha haya.

Ndugu na dada zangu, hebu endelea kuwa na subira na uwe na pumziko la kujua kwamba punde si punde ukombozi kutokana na vazi hili la majonzi waja.. Basi tusisukumwe huku na huko na ulimwengu huu, bali tuweke guzo na kutoa mioyo yetu kwa upendo wake Kristo. Hebu tudumishe macho yetu kwa Yesu—huku tukisubiri kwa uvumilivu, na kuingia zaidi katika upendo wake Mungu, kufanya bidii kuokoa waliopotea, tuwe macho na tudumishe umakini kila siku kwa mambo hayo. Basi tusijisalimishe katika hali ya kupoteza tumaini na kufa moyo, bali tusubiri kwa uvumilivu—kwa maana kuja kwa Bwana Yesu kumekaribia sana. ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana